
**Arafa ya Sera**
Nambari 45 Juni 2015

REPUBLIC OF KENYA

Mashirika Husika: Shirika la Taifa la Idadi ya Watu na Maendeleo, Wizara ya Afya, Chuo cha Masomo na Utafiti wa Idadi ya Watu, na Taasisi ya Kumbukumbu za Idadi ya Watu.

# Upangaji Uzazi na Afya ya Uzazi: Wanaume Wako Wapi?

Kuhusisha wanaume na mpango wa uzazi na afya ya uzazi ni muhimu kwa kukuza afya ya jamii. Nchini Kenya, kuhusishwa kwa wanaume kumekua chini sana, ukichangia utumizi mdogo wa huduma za upangaji uzazi na kusababisha vifo vingi vya mama wajauzito na watoto nchini.



**Hii arafa ya sera inasisitiza matokeo muhimu ya utafiti huu na kupendekeza kuwa wananchi wazidi kufahamishwa zaidi kuhusu umuhimu wa mpango wa uzazi na afya ya uzazi, kuchunguzwa upya majukumu ya jinsia tofauti, na kufanya mpango wa uzazi na huduma za afya ya uzazi ziwe za kirafiki kwa wanaume.**

Kuzingatia hali hii, Utafiti wa Kitaifa wa mwaka 2014 kuhusu Kuhusishwa kwa Wanaume Kwa Mipango ya Uzazi na Afya ya Uzazi ulitafiti hali inayozuia wanaume kuhusika na upangaji uzazi kwa lengo la kubuni mikakati ya kuboresha kuhusishwa kwa wanaume. Hii arafa ya sera inasisitiza matokeo muhimu ya utafiti huu na kupendekeza kuwa wananchi wazidi kufahamishwa zaidi kuhusu umuhimu wa mpango wa uzazi na afya ya uzazi, kuchunguzwa upya majukumu ya jinsia tofauti, na kufanya mpango wa uzazi na huduma za afya ya uzazi ziwe za kirafiki kwa wanaume.

## Kwa Nini Wanaume Walengwe?

Mpango wa uzazi na utaratibu wa afya ya uzazi umeundwa kuhudumia wanawake, ijapokua kuhusishwa kwa wanaume imetambuliwa kuwa muhimu kwa afya ya jamii. Kwenye mkutano wa kimataifa wa mwaka 1994 wa idadi ya watu na maendeleo, kuhusishwa kwa wanaume ilielezwa kuwa kuwajibikia kwa wanaume katika masuala ya ngono na tabia ya uzazi ambayo inaunga mkono wanawake kutumia mpango wa uzazi, huduma ya afya ya wanawake na watoto, na kutumia njia za wanaume za kuendeleza kupanga uzazi.[1]

Utafiti Kenya umeonyesha kuwa kuhusishwa kwa wanaume na mpango wa uzazi na mambo ya afya ya uzazi ni nadra.[2] Utafiti wa Idadi ya watu na Afya wa mwaka 2008-09 (KDHS) ulifichua kuwa wanaume wengi hawaungi mkono wanawake kutumia mpango wa uzazi. Wanaume wawili kati ya watano waliamini kuwa wanawake wakitumia mpango wa uzazi utawafanya wawe makahaba na mwanaume mmoja kati ya tano walisema kuwa upangaji uzazi ni jambo la wanawake. Pia, baadhi ya maswala yaliosababisha wanawake kuzaa nyumbani ni kwamba waume wao walipinga wake zao kuzaa katika kituo cha afya.

Kenya bado ingali nyuma katika mambo mengi ya afya ambayo ingekuwa bora zaidi ikiwa wanaume wangehusishwa. Ingawaje matumizi ya mbinu mbali mbali za upangazi wa uzazi imeongezeka na wastani wa idadi ya watoto wanaozaliwa na kila mwanamke imepunguka kati ya mwaka 2008 na 2014, wanawake bado wanazaa watoto wanne au zaidi kwa wastani katika zaidi ya nusu ya kaunti arubaini na saba za Kenya.[3] Zaidi ya hapo, vifo vinavyohusika na uja uzito, pamoja na vifo vya watoto, vinaweza kuzuiwa kwa kuongeza matumizi ya mbinu za kupanga uzazi, huduma za afya kwa akina mama wajawazito, na kutumia wakunga waliohitimu.

## Jitihada Nchini Kenya Kuwahusisha Zaidi Wanaume

Sera ya idadi ya watu na maendeleo Kenya inatambua kuwa kutojihusisha sana kwa wanaume na upangaji uzazi na afya ya uzazi ni kikwazo kwa kupunguza mwendo wa kukua kwa idadi ya watu kwenda sambamba na rasilimali zilizoko nchini.[4] Sera hii inapendekeza kujumuishwa kwa sekta mbali mbali, kama vile afya, jinsia, idadi ya watu, na mawasiliano kuendeleza kuhusika zaidi kwa wanaume. Sera ya kitaifa ya afya ya uzazi inatambua kutohusishwa sana kwa wanaume kama kikwazo kwa kufanikiwa kwa kijinsia kwa kutumia huduma ya afya, uzazi, na kwa hivyo kupatia kipaumbele na kuhusisha wanaume kwa utaratibu wa afya ya uzazi.[5] Jitihada mashinani za kuhusisha wanaume zaidi imekua kwa miradi midogo ya wizara ya afya na mashirika yasiyo ya serikali. Kujulisha sera na taratibu zijazo, shirika la idadi ya watu na maendeleo (NCPD) ilifanya utafiti wa kitaifa kuhusu wanaume kuhusishwa na mpango wa uzazi ili kuelewa vizuri sababu za wanaume kutojihusisha sana na upangaji uzazi kupitia mahojiano na mazungumzo ya vikundi. Utafiti ulikadiria elimu ya jamii dhana na fikra kuhusu upangaji wa uzazi na afya ya uzazi.[6]

## Utambuzi wa Jamii Kuhusu Kuhusiswa kwa Wanaume

Utafiti uliofanywa juu ya kuhusishwa kwa wanaume na mpango wa uzazi ulionyesha utambuzi hasi kuhusu kuhusishwa kwa wanaume katika mpango wa uzazi na afya ya uzazi kwenye kaunti nyingi nchini Kenya. Changamoto za kiafya, matukio na kuelewa vibaya, utamaduni na dini zinachangia kuunda mitazamo ya jamii. Kwenye kaunti nyingi kama vile Kisumu, Wajir na Kitui, wanaume walidokeza kuwa njia za kupanga uzazi zinasababisha kutokwa damu nyingi sana, kufura miguu na kuongezeka uzito kwa wanawake. Pia wanaume walisema kuwa hizi njia za kupanga uzazi zinafanya wanawake wawe tasa, wapate kansa na kukosa nyege na kwa hivyo wanaume kupinga wanawake kutumia njia za kupanga uzazi. Kwa kaunti nyingi, kama vile Pokot Magharibi, Migori na Kajiado, utunzaji wa watoto wadogo na utumiaji wa njia za kupanga uzazi inatazamwa kama wajibu wa wanawake hivikwamba wanaume ambao wanajihusisha na mambo haya wanachukuliwa kuwa hawana usemi katika familia na jamii. Vile vile, dini nyingine zinaunga mkono uzazi wa majira na kutumia njia ya asili kupanga uzazi kama vile kuzuia kufanya ngono kwa muda, lakini wanaume wanapinga njia za kupanga uzazi wakizichukulia kuwa zinawafanya wanaume na wanawake wawe tasa.

> *'Tunasikia kuwa kupanga uzazi inaharibu miili ya wanawake. Ati kuna njia zingine za kupanga uzazi zikitumiwa na wanawake zinawafanya wanenepe, je hii ni kweli?'*
>
> **Wanaume – Kisumu Kaunti**

Miongoni mwa vijana wa umri 15 – 24, utafiti ulipata ongezeko la ufahamu kuhusu haja ya wanaume kuhusishwa na upangaji uzazi kwa sababu za kiuchumi na uchache wa rasilimali kama ardhi. Waliojibu maswali ya utafiti katika kaunti za Vihiga, Kitui na Nyeri waliunga mkono upangaji uzazi kwa sababu walisema kwamba unazuia umaskini na changamoto zinazohusishwa na familia kubwa. Wanaume wengine walitaja faida ya mpango wa uzazi kwa kuimarisha afya ya wanawake na watoto.

> *'Shamba zetu ni ndogo mno na ukizaa watoto wengi, kama wavulana tano na uko na hekari moja ya ardhi, wakiwa wakubwa watajenga na kupanda chakula wapi ili kulisha familia zao?'*
>
> **Vijana – Kaunti ya Vihiga**

## Wajibu wa Wanaume na Malengo Yao

Licha ya utambuzi wa maoni hasi, utafiti uliofanywa ulipata kwamba wanaume wanahusika pakubwa kwa kuimarisha afya ya uzazi na jamii. Wanaume wengi wanaunga mkono mpango wa uzazi na afya ya uzazi kifedha kwa kutoa pesa za chakula, kugharamia huduma za afya na usafiri wa wanawake na watoto. Wanaume wengine katika sehemu kama Meru na Machakos waliripoti kuhimiza bibi zao kutumia huduma hizi.

Kuhusu wajibu wa wanaume, katika theluthi moja za kaunti, wanaume wengi waliripoti kuwa wangependa kuandamana na wake wao kwa vituo vya afya kupata huduma. Hawa wanaume walisema kuwa wangependa kusaidia wake wao na kazi za nyumbani na kuhimili matatizo ya kiakili kwa wanawake wajawazito kabla na baada ya kuzaa. Wengi wa wasichana wachanga kati ya umri 15 – 24 pia waliunga mkono maoni haya. Katika zaidi ya nusu za kaunti, wanaume wengi walisema kuwa wangependa kuelimisha wanaume wenzao, hasa wale wanao jiandaa kuoa, kuhusu mpango wa uzazi na afya ya uzazi.

*'Watoto ni wa mume na mke na jukumu la kuwalea ni lao wote'.*

**Wasichana wachanga – Kaunti ya Machakos**

## Vizuizi kwa Wanaume Kuhusika

Vizuizi kwa wanaume kuhusika na mpango wa uzazi na afya ya uzazi vilivyotambuliwa katika utafiti vinaweza kubainishwa kama vizuizi vinavyohusiana na mtu binafsi, jamii, huduma za afya na vizuizi vya sera.

Kwa mtu binafsi, kizuizi kikubwa ni habari na elimu pungufu au potovu kuhusu mpango wa uzazi na afya ya uzazi. Vizuizi vingine ni ukosefu wa mawasiliano kati ya mume na mke, ulevi, mabwana kutokuwepo nyumbani na ushawishi kutoka kwa marika wa mume. Hasa mawasiliano duni kati ya mume na mke huchangia utumizi mdogo wa njia za kupanga uzazi zinazopatikana kwa wanaume (kondomu na kuhasi). Ushawishi wa marika na familia unawazuiya wanaume kusindikiza wake wao kwa vituo vya afya na kutunza watoto nyumbani. Katika theluthi mbili za kaunti, wanawake wachanga kati ya umri 15- 24 walisema kuwa mabwana wao hawashindi nyumbani kwa sababu ya kikazi au shuguli za kijamii na kwa hivyo walikuwa na muda mfupi wa kuzungumza mambo ya mpango wa uzazi na aya ya kina mama. Kwa wanaume wengi katika kaunti zaidi ya ishirini na tano waliripoti kuwa hawazungumzi na wake wao kuhusu afya ya uzazi kwa sababu hilo jambo ni la wanawake. Utafiti huu pia ulionyesha kwamba wanawake wa umri mkubwa huandamana na wanawake wajawazito kwa vituo vya afya badala ya wanaume wao.

Vizuizi vya jamii ambavyo vinazuia wanaume kujihusisha na mpango wa uzazi na afya ya uzazi ni kutamani watoto wengi, ndoa ya wake wengi, kupinga njia za kupanga uzazi na kupendelea watoto wa kiume. Hili lilikuwa jambo hasa katika kaunti zilizoko maeneo ya Nyanza, Western, Central, Rift na North Rift.

*'Wanaume wetu wanaamuka mapema kwenda kufanya kazi. Wakitoka kazini wanaenda kunywa pombe ya kienyeji na wakija nyumbani ni walevi kiasi ya kwamba hatuwezi kuongea chochote'.*

**Wanawake – Kaunti ya Bungoma**

Katika kaunti zilizoko maeneo ya Pwani na Kaskazini Mashariki, dini ilichangia sana kupinga matumizi ya mpango wa uzazi katika kaunti nyingi. Kanuni za jamii kuhusu wajibu wakijnsia ulizuia wanaume kuhusika na utunzaji wa watoto, kusaidia kazi za nyumba na kutumia huduma za kupanga uzazi.

Nchini Kenya, kinachowazuia wanaume kutumia huduma za kupanga uzazi ni kukosekana kwa wahudumu wanaume. Katika kaunti zote, wanaume waliashiria kuwa hawaendi kwa vituo vya afya kwa sababu hawataki kuhudmiwa na wahudumu wa afya wa kike. Vizuizi vingine katika vituo vya afya vilikuwa huduma zinazotolewa polepole, kungojea huduma kwa muda mrefu, wahudumu wasiokuwa na urafiki, kukosekana kwa siri, na upungufu wa mbinu tofauti za upangazi uzazi kwa wanawake na wanaume.

*'Mpango wa uzazi ni jambo la mwanamke kwa sababu wanaume hawakuhusishwa mwanzoni. Wahudumu wa afya wanashughulika sana na afya ya wanawake na watoto kwa sababu ni jambo la wanawake, na wanaume wanachukua hilo jambo hivyo na wahudumu wa mpango wa uzazi na afya ya mama na watoto ni wanawake. Sisi wanaume tunaogopa kuuliza kuhusu mpango wa uzazi kwa sababu ni jambo la wanawake'.*

**Wanaume– Kaunti ya Embu**

Ijapokuwa kuna sera zinazounga wanaume kuhusishwa na afya ya uzazi, mikakati ya kushugulisha wanaume haijasambazwa kikamilifu katika kaunti wala hazijaungamanishwa katika mipango za kaunti. Zaidi ya hapo, utafiti ulipata kuwa fahamu kuhusu sera za mpango wa uzazi na afya ya uzazi zilikuwa chini miongoni mwa wahudumu wa afya, hasa kwenye secta ya banafsi.

NCPD ni Shirika la Serikali linalobuni na kuimarisha sera za idadi ya watu na kushirikisha shughuli zinahusiana kwa ustawi wa maendeleo nchini Kenya.

**NCPD**

**Baraza la Kitaifa la Idadi ya Watu na Maendeleo**

S.L.P 48994 - GPO,
Nairobi 00100, Kenya

Simu: 254-20-271-1600/01

Kipepesi: 254-20-271-6508

Baruapepe: info@ncpd-ke.org

**www.ncpd-ke.org**

Jarida hili limetolewa kwa hisani ya Watu wa Marekani kupitia Shirika la Ustawi wa Maendeleo ya Kimataifa (USAID) chini ya mkataba wa Mradi wa IDEA (No. AID- 0AA-A-10-00009). Baraza la Kitaifa la Idadi ya Watu na maendeleo -NCPD linawajibika kwa yaliyomo kwenye jarida hili na hayaangazii maoni ya shirika la USAID wala Serikali ya Marekani.

## Vidokezi na Mapendekezo

Dhana potevu kuhusu mpango wa uzazi kwa sababu ya shaka au masikitiko ya kiafya, matukio na uwongo, au utamaduni na dini inahitaji elimu zaidi kwa umma kuhusu mpango na afya ya uzazi. Ingawaje wanaume wanahusishwa sana na kutoa pesa, wengi wangependa kuhusishwa zaidi hasa wakati wa uja uzito na baada ya kuzaliwa kwa mtoto. Kuchukuwa fursa hii kutahitaji kubadilisha kanuni za jamii ambazo zinazuia wanaume kuhusika sana na mambo ya afya ya uzazi. Kwa sababu huduma za afya nchini zimegatuliwa kwa serikali za kaunti, mbinu za kuhusisha wanaume zaidi katika hizi huduma zinahitaji kungatuliwa kwa kaunti zote.

## Shirika la idadi ya watu na maendeleo inapendekeza yafuatayo:

1. **Kuzidisha elimu ya umma kuhusu mpango wa uzazi na afya ya uzazi:** Shirika la idadi ya watu na maendeleo pamoja na wizara ya afya ikuze taarifa ya kina kuelimisha wanaume na wanawake. Hizi shirika mbili zifanye kamppeni ya uma kote nchini kuongeza kuhusihswa kwa wanaume kwa kutumia habari mwafaka katika kila kaunti kuhusu vizuizi vinavyochangia watu kutotumia huduma za mpango wa uzazi kama afya na matukio na kuelewa mambo vibaya.

2. **Kuzungumzia kanuni za kijinsia katika jamii:** Shirika la idadi ya watu na maendeleo, bodi ya wakurugenzi ya kijinsia na tume ya kijnsia itengeneze mikakati ya kutoa changamoto za kijinsia ambazo zinazuia wanaume kuhusishwa na mpango wa uzazi na afya ya uzazi. Kwa matokeo mazuri, mikakati ya utetezi ichunguze changamoto za kila kaunti, na ambapo inawezekana, itekelezwe pamoja na jitihada na elimu ya umma iliyoelezwa mbeleni.

3. **Kuvifanya vituo vya afya viwe vya kirafiki kwa wanaume:** Kuvutia wanaume zaidi kutumia huduma za mpango wa uzazi na afya ya uzazi, wizara ya afya iongeze juhudi kwa kuajiri wahudumu wa afya wa kiume zaidi, kupunguza muda wa kungojea huduma, kuendeleza zaidi mwendo wa kutoa huduma, kutia moyo wahudumu wawe wazuri kwa wanaume, kutoa huduma kwa faragha, kutumia wanaume wanaojitolea kwa hiari kutoa huduma kwa jamii, na kuhakikisha kwamba kuna njia nyingi za kutosha za upangaji uzazi kwa wanaume na wanawake katika vituo vyote vya afya.

4. **Kugatuliwa kwa sera za kitaifa kwa kila kaunti:** Sera kuhusu mpango wa uzazi na afya ya uzazi zigatuliwe kulingana na hali ya kila kaunti. Kufanikisha hii, Shirika la idadi ya watu na maendeleo na wizara ya afya itahimiza secta ya afya na mpango katika kaunti ili zielewe madhumuni ya sera za kitaifa kabla ya kuzijumuisha katika mikakati ya mipango . Hizi sera zikishatengenezwa, kila wizara ya afya ya kaunti itahamasisha wahudumu wake wa afya kuhusu sera hizi na mikakati.

Kutekeleza mapendekezo yaliyotajwa itachangia sana wanaume kuhusika na upangaji uzazi na afya ya uzazi nyumbani na katika jamii pamoja na kutumia huduma hizi katika vituo vya afya. Hii itachangia kuboresha afya ya wanaume, wanawake na watoto.

## Kumbukumbu

[1] United Nations Population Fund (UNFPA), *Programme of Action of the International Conference on Population and Development* (New York: UNFPA, 1994).

[2] Kenya National Bureau of Statistics, National Council for Population and Development, and ICF Macro, *Kenya Demographic and Health Surveys* (Calverton, Maryland, USA: ICF Macro, 1998, 2003, and 2009).

[3] KNBS, NACC, KEMRI, NCPD, and ICF Macro, *Kenya Demographic and Health Survey 2014* (Calverton, Maryland, USA: ICF Macro, 2015).

[4] NCPD, *Population Policy for National Development* (Nairobi, Kenya: NCPD, 2012).

[5] Ministry of Health, *National Reproductive Health Policy – Enhancing Reproductive Health Status for All Kenyans*. (Nairobi, Kenya: MOH, 2012).

[6] NCPD, *National Survey on Male Involvement in Family Planning and Reproductive Health in Kenya* (Nairobi, Kenya: NCPD 2014).

© 2015 Baraza la Kitaifa la Idadi ya Watu na Maendeleo